

## **TANGAZO LA NAFASI ZA UKUFUNZI WA MUDA (PART TIME TRAINER)**

Idara ya Mafunzo ya Ualimu kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA) imeandaa mafunzo kwa walimu wa masomo ya Sayansi na Hisabati wanaofundisha Kidato cha kwanza (form I) na Kidato cha pili (form II) chini ya mradi wa ZISP. Mafunzo hayo yanategemewa kutolewa katika Vituo vya Walimu Unguja na Pemba kwa muda wa siku 160 na kuendeshwa siku mbili tu kwa wiki.

Hivyo Idara inatangaza nafasi za ukufunzi wa muda (part time trainer) watakaotoa mafunzo katika Vituo vya Walimu Unguja na Pemba.

Sifa za waombaji ni kama zifuatazo:

- a. Awe Mzanzibari Mkaazi.
- b. Awe mwalimu ambae amesomea angalau stashahada (Diploma) au zaidi na na uzoefu wa kusomesha si chini ya miaka 10 katika masomo ya Sayansi, Hisabati, English na TEHAMA (Mathematics, Biology, Chemistry, physics, English and ICT) katika madarasa ya sekondari au vyuo vya ualimu.
- c. Awe na uwezo wa kufundisha masomo hayo kwa kutumia lugha ya Kiingereza kwa ufasaha.
- d. Awe tayari kufanya kazi katika mazingira magumu.
- e. Awe anajiamini, kujituma na kufuata maadili ya ualimu.
- f. Awe tayari kufanya kazi ndani ya siku za kazi na za mapumziko.
- g. Aweze kuwasiliana kwa kutumia lugha ya Kiingereza.
- h. Mwenye uwezo wa kutumia computer katika program za MS word, Excel na PowerPoint atapewa kipaumbele.

Muombaji anatakiwa kuandika barua ya maombi kwa Mkurugenzi Idara ya Mafunzo ya Ualimu, na kuiwasilisha ofisi ya Idara ya Mafunzo ya Ualimu mtaa wa Majestic jirani na jengo la Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu Zanzibar. Kwa waombaji kutoka Pemba wawasilishe barua zao Ofisi kuu ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Pemba katika kitengo cha Mafunzo ya Ualimu, Chake Chake Pemba.

Barua za maombi ziambatanishwe na:

- a. Kivuli cha cheti cha kuzaliwa.
- b. Vivuli vya vyeti vya kumaliza masomo.
- c. Karatasi ya maelezo yasiozidi kurasa moja kwa lugha ya kiingereza na yaliyochapwa yanayoeleza dhamira na sababu za kuomba kwake kazi hiyo.

d. CV.

e. Kivuli cha Kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi.

Mwisho wa kutuma maombi ni tarehe 24/11/2017 saa nane mchana.

**TANBIHI:**

- a. Mouombaji aainishe katika barua yake ya maombi somo atakalolifundisha.
- b. Tangazo hili pia linapatika katika tovuti ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali –Zanzibar “[www.moez.go.tz](http://www.moez.go.tz)”